

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

**Simu:** +255 753 545 294  
+255 784 487 658



**S.L.P. 72**  
**KYERWA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**YAHUSU VIFO VYA WANAFUNZI WANNE KWA AJALI YA RADI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa inasikitika kutoa taarifa za kusikitisha za vifo vya watoto wanne kwa ajali ya Radi. Tukio hii lilitokea katika kitongoji cha Kihinda, kijiji cha Kihinda kata ya Kibingo mnamo tarehe 05/04/2018 majira ya saa 11 za jioni wakati mvua kubwa iliyoambatana na radi iliponyesha katika eneo tajwa. Waliofariki ni **Reminatha Venant miaka 13 (Ke)** wa darasa la tano, **Imani Venant miaka 5 (Me)** wa darasa la awali, **Innocent Robert miaka 10 (Ke)** wa darasa la tatu na **Eliakim Evarista miaka 10 (Ke)** wa darasa la pili wote katika shule ya msingi Kihinda. Aidha watoto hawa wawili ni utoka katika familia moja na wawili ni wa familia tofauti. Uongozi wa Wilaya ukiongozwa na Mkuu wa Wilaya walifika kuthibitisha tukio hilo na kutoa salamu za pole kwa wafiwa.

Mkuu wa Wilaya, **Kanali Mstaafu Shaban Lissu** kwa niaba ya Serikali ametoa salamu za rambirambi na kutoa pole kwa wafiwa wote na kuwaomba wawe na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu kwao na kwa serikali. Aidha amewasihi kudumisha amani na kuacha kufikiria mambo ya kishirikina kitu ambacho kinaweza kuhatarisha amani. **"Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi"**

Imetolewa na



Golden Nzalalila  
**KAIMU AFISA HABARI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**

**KYERWA**